

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA**



**TAARIFA KWA UMMA**

Desemba 26, 2022

[www.ludewadc.go.tz](http://www.ludewadc.go.tz)

**LUDEWA, NJOMBE- TANZANIA**

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mhe. Andrea Tsere katika kuadhimisha sherehe za Krismasi na Mwaka mpya ameongoza wataanzania kusherehekea sherehe hizo kwa kushiriki shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na uhamasishaji wa kushiriki shughuli za kimaendeleo pamoja na kuhamasisha wananchi ufanyaji usafi wa mazingira.

Zoezi hilo limefanyika katika kata ya Lupingu alipoalikwa Kama mgeni rasmi katika siku ya Desemba 24, 2022.

Aidha tukio hilo lilitanguliwa na tukio muhimu jingine ambapo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratias Desemba 23, 2022 alipokea vifaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na mikoba Maalumu ya kutunzia kumbukumbu kwa ajili ya Waheshimiwa Madiwani wa Kata zote na Wakuu wa Divisheni wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kutoka kwa wadau wa maendeleo waishio nje ya Tanzania na ndani ya nchi wanaojulikana kwa utambulisho wa LUPINGU DIASPORA.

Wakati akikabidhi vifaa hivyo mkuu wa msafara wa Lupingu Diaspora ndg. Melchior Ndofi alisema kuwa ikiwa ni sehemu ya kutambua kazi kubwa inayofanywa na serikali ya awamu ya sita nao kama wadau wa maendeleo kutoka Wilaya ya Ludewa wameona vyema kurudisha fadhila hizo wilayani Ludewa kwa kutoa michango mbalimbali kwa ajili kuunga mkono shughuli za maendeleo wilayani Ludewa.

Aidha Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa alisema kuwa anatambua mchango mkubwa unaofanywa na Lupingu Diaspora kwa ushiriki wao katika shughuli mbalimbali za maendeleo kwenye Wilaya ya Ludewa kwani wamekuwa chachu ya kuhamasisha maendeleo hasa kwenye kata ya Lupingu.

Lupingu Diaspora kuelekea sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya wanaadhimisha sikukuu hizo katika kata ya Lupingu kwa kushiriki shughuli mbalimbali za maendeleo pamoja na michezo ikiwemo kuogelea, kukimbia, mganda, kihoda nk.

**Chrispin B. Kalinga**

**Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini**

*Ludewa ya Utalii, Uchumi wa Chuma na Mkaa ya Mawe kwa Maendeleo Yetu.*